BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Kwanza – Tarehe 15 Disemba, 2021.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 18 Septemba, 2021.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Serikali Kuhusu Ripoti ya Tano ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili kwa mwaka 2020/2021.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Ripoti ya Tano ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili kwa mwaka 2020/2021.

MASWALI:

<u>Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:</u>

35. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.

Ili kutanua uwakilishi wa wanawake katika vyombo tofauti vya maamuzi, Serikali iliridhia kuwepo kwa asilimia arubaini ya viti vya majimbo, sawa na viti ishirini, kama viti maalum vya wanawake bila kuzingatia wanawake wangapi wameshinda katika viti vya majimbo. Hata hivyo, katika Baraza la Kumi la Wawakilishi kuna wanawake kumi na nane tu wa viti maalum badala ya ishirini kama takwa la kifungu cha 67 (1) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

(a) Je, kwa nini Serikali imewanyima wanawake viti vyao viwili na kukivunja kifungu cha Katiba ya Zanzibar kilichoruhusu viti maalum.

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani kulitatua hilo na lini wanawake watarejeshewa viti vyao viwili katika Baraza la Wawakilishi kama haki yao ya msingi na ya kikatiba.

<u>Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:</u>

88. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Mabadiliko ya Tabia Nchi yamekuwa ni moja kati ya majanga yanayoikumba dunia na kupelekea baadhi ya maeneo ya kilimo kuvamiwa na maji ya bahari.

(a) Je, ni lini hatua za kudhibiti maji ya bahari yanayoathiri wakulima wa bonde la wapape zitachukuliwa ili kuwapa unafuu wakulima hao.

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kinaweza kutatua tatizo hilo.

<u>Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>

161. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Meli ya Spice Islander ilizama tarehe 10/9/2011 na kupoteza maisha ya baadhi ya wasafiri na baada ya kadhia hiyo Serikali iliwashtaki wafanyakazi wanne wa Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa kosa la uzembe uliosababisha ajali hiyo. Kesi hiyo imeendeshwa kwa karibu miaka 10 huku wafanyakazi hao wakilipwa nusu mshahara, hata hivyo wafanyakazi hao walishinda kesi hiyo katika ngazi zote za Mahakama hadi Rufaa.

Baada ya kumalizika kesi hiyo wafanyakazi hao walitakiwa kurejeshwa kazini na kulipwa mafao yote kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma. Pamoja na kurejeshwa kazini, ni wafanyakazi wawili tu ndiyo waliostahili kuwepo kazini na wawili umri wa kustaafu ulishafikia, hivyo walistahiki kulipwa mafao yao na nusu mshahara wao waliokuwa hawalipwi kwa kipindi chote cha kesi.

(a) Kwa kuwa Sheria ya Utumishi wa Umma inatambua haki za kulipwa stahiki zao hizo Je, ni lini Serikali itawalipa malipo yao hayo.

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kilistahili kulipwa wafanyakazi hao wanne.

<u>Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:</u>

109. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji:

(a) Wizara imefanya tathmini ya Wanadiaspora wangapi waliobobea katika fani za umeme, elimu, uhandisi, maji, na mazingira, ambao asili yao ni kutoka Zanzibar.

(b) Je, Wizara inawapa mashirikiano gani Wanadiaspora hao ili kuona kwamba wanatusaidia kwa mnasaba wa taaluma zao.

<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>

145. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) -

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Makusanyo ya vibali vya mali zisizohamishika vinalipwa katika Idara ya Misitu kupitia Account namba yao, lakini kwa Halmashauri makusanyo yanaenda Hazina Kuu na ardhi wakati wa kurudi fedha huwa hazipatikani zote.

Je, ni sababu gani inayopelekea kukosekana kwa fedha zote wakati yale ni makusanyo ya Wilaya husika.

<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>

39. MHESHIMIWA HUDHAIMA MBARAK TAHIR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kukamilisha ahadi kwa vijana kupitia Ilani ya Uchaguzi ya 2020-2025 inalazimika kutenga fedha kupitia mapato ya Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri kwa asilimia 4 kwa ajili ya kuwasaidia vijana wa makundi tofauti kujiendeleza kupitia miradi yao.

(a) Je, kwa kipindi cha miezi mitatu ya utekelezaji wa bajeti ya 2021-2022, ni kiasi gani kwa Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri zote zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ahadi kwa vijana.

(b) Je, kwa kuzingatia mchanganuo kwa kila Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri, ni vijana au makundi ya vijana mangapi yamefaidika na fedha hizo kwa Unguja na Pemba.

(c) Je, kuna taaluma gani wanazopata vijana kabla ya kupatiwa fedha, ili kupata ufanisi wa utekelezaji wa miradi na biashara zao.

<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>

9. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) -

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Redio na televisheni ni mdomo muhimu wa Serikali yetu.

Je, Serikali haioni kuwa iko haja ya kuyafanyia ukarabati majengo yake ya ZBC TV na ZBC Redio walau kwa hatua ya kuyapaka rangi tu ili kuonyesha umuhimu wa majengo hayo.

76. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa viwanja vya mipira vilivyomo ndani ya Wilaya na Shehia viko chini ya Halmashauri za Wilaya husika.

(a) Je, ni utaratibu gani unaotumika wa uvitengeneza viwanja hivyo.

(b) Kwa kuwa uwanja wa mpira wa Konde kunahitajika kuwekwa sawa na kuwekewa vikalio. Je, ni lini uwanja huu utarekebishwa na kurudi katika uhalisia kama vilivyo viwanja vyengine vya mpira.

<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>

13. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Katika suala la upatikanaji wa huduma ya umeme nchini kote, suala la uwepo wa "transformer" ni muhimu sana kwa ajili ya utowaji wa huduma hiyo.

(a) Je, Serikali inanunua wapi bidhaa hii ya "transformer".

(b) Je, ni vigezo gani vinavyochukuliwa katika kuhakikisha "transformer" zinazonunuliwa ni zenye ubora zaidi.

58. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa miaka miwili mtandao wa mabomba ya maji unaotoka Kiweshangwe kuelekea Nungwi umekuwa na tatizo kubwa la uvujaji maji hasa maeneo ya shehia ya Tazari.

(a) Je, Mamlaka ya Maji (ZAWA) ina mpango gani wa kuyaziba mabomba hayo.

(b) Kwa kuwa mabomba haya yanaonekana ni sugu kimuundo. Je, ni lini Serikali itayabadilisha ili kuondokana na upotevu wa huduma hii muhimu kwa jamii.

<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>

14. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Eneo la Shehia ni eneo maarufu sana kwa kilimo cha mpunga wa kumwagilia unaolimwa sana na wakulima wa juu. Hata hivyo, wakulima wote hao wanakabiliwa na changamoto za ubovu wa miundombinu ya umwagiliaji, uhaba wa mbolea, dawa za kuulia magugu na pembejeo nyengine hali ambayo imepunguza sana upatikanaji wa nafaka ya mpunga.

(a) Kwa kuwa eneo hilo kwa miaka yote linatambulika kwamba ni eneo la kilimo, Je, Serikali haioni kwamba wakati umefika kwa eneo lote la Bumbwisudi kulifanya kuwa eneo la kilimo cha umwagiliaji.

(b) Ni lini Serikali itapeleka wataalamu wa kutosha wa kilimo ili kuwasaidia wakulima wa eneo hilo na kuondoa changamoto zilizojitokeza.

<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>

18. MHESHIMIWA HABIBU ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) -

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

Moja kati ya safari zisizohitaji kubahatisha ni safari za anga. Hata hivyo, tunapenda kufahamu kutoka kwako.

(a) Ni ipi mipango ya Serikali kupitia Wizara yako katika uwekezaji wa ndege zenye ubora na uhakika Zanzibar.

(b) Je, ni lini Wazanzibari watapata ndege za safari za uhakika kuliko kuendelea kusafiria kwa ndege ndogo sana kama vile Auric, Coastal na nyenginezo.

<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>

5. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa hadi leo kilimo kinaendelea kuwa uti wa mgongo wa uchumi wa Zanzibar. Na kwa kuwa hadi leo bado Wazanzibari tunaendelea kutumia kilimo asilia huku tukiwa na uchache wa wataalamu pamoja na upungufu au kukosekana kabisa kwa vituo vya utafiti wa kilimo vinavyojishughulisha na uzalishaji wa mbegu bora za kilimo pamoja na kufanya tafiti mbali mbali za mazingira na wadudu waharibifu wa mazao.

(a) Je, ni lini Chuo Kikuu cha Taifa SUZA kitaanzisha Kitivo cha Sayansi ya Kilimo (Faculty of Agricultural Science) ili kuongeza wataalamu katika fani mbali mbali za kilimo.

(b) Ni lini SUZA itaanzisha “Faculty of Agricultural Mechanics Pemba Branch” ili kutoa wataalamu watakaotengeneza zana za kilimo zinazoendelea kuharibika siku hadi siku kisiwani Pemba.

106. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Taaluma ya ujasiriamali kwa sasa imekuwa ni jambo

lisiloepukika katika kuwawezesha wananchi kujitegemea kiuchumi na kuondoa ukakasi wa ukosefu wa ajira.

Je, Wizara yako haioni kwamba ipo haja ya kuliingiza somo hili kwenye mtaala wa kufundishia. Licha ya kwamba somo hili limekuwa likifundishwa katika vyuo na taasisi mbali mbali.

<u>Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:</u>

1. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

   Kwa kuwa Kituo cha Afya kilichopo katika kisiwa cha Kojani tayari kimeshajengwa jengo la nyumba ya daktari. Na kwa kuwa mazingira ya jengo hilo sio rafiki kwa kuishi mtumishi wa umma.

   Je, ni lini Serikali italifanyia ukarabati mkubwa jengo hilo ili lifikie kiwango cha kuishi daktari wa kituo hicho.

<u>Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:</u>

170. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

   Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikitoa bei elekezi ili kumlinda mwananchi wake.

   (a) Je, ni mamlaka gani inayosimamia utekelezaji wa bei elekezi hapa nchini.

   (b) Je, Mamlaka hizo zinawajibika kwa kiasi gani.

   (c) Kuna taarifa ya wafanyabiashara wanaokiuka bei elekezi, Je, mamlaka husika inazo taarifa hizo.

<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>

200. MHESHIMIWA SAADA RAMADHAN MWENDWA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na

Mambo ya Kale:

Kwa kipindi kirefu sekta ya utalii hasa katika eneo la Mji Mkongwe imekuwa ikiingiza pato kubwa nchini. Hata hivyo, pamoja na sekta hiyo kuingiza kipato kikubwa bado hakuna utaratibu maalum kwa wanawake wa Mkoa wa Mjini Magharibi kuweza kufaidika na sekta hiyo ya utalii.

(a) Kwa kuwa wanawake ni makundi muhimu katika maendeleo ya nchi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwashirikisha wanawake ili wafaidike na sekta ya utalii.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha utalii wa ndani.

<u>Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:</u>

41. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Uzoefu unaonesha kuwa hadi hivi sasa maeneo mengi ya Serikali hayana hati miliki, hali inayopelekea maeneo hayo kuvamiwa na wananchi kwa shughuli zao za kijamii ikiwemo kilimo na kujenga nyumba za makaazi.

(a) Je, Serikali inalitambua swali hili.

(b) Ni sababu gani zinazopelekea hadi sasa maeneo hayo kutopatiwa hati miliki hasa ukizingatia umuhimu wa kupatikana kwa hati hizo.

III. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>

<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>

Taarifa ya Serikali Kuhusu Ripoti ya Tano ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili kwa mwaka 2020/2021.

Zanzibar,
15 Disemba, 2021.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.